

Pambazuko

Toleo Namba 0038

Jumatatu Mei 15-21, 2023

Madaktari wafura' mwenzao kuuawa

Uk. 7



Miradi ya PPP kuifungua nchi

● *Msisitizo sekta binafsi kukaa tayari*

Chozi la Kikwete kumlilia Membe

Uk. 5

JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Tahariri

**Nenda Salama Membe.
Pambazuko tunakulilia!**



:1953 – 2023:

POLE FAMILIA YA MEMBE ...



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe akimpa pole Dorcas Membe, kwa kufiwa na mumewe Bernard Membe wakati alipofika nyumbani kwake Mikocheni, Dar es Salaam. Membe aliyefariki dunia Ijuma iliyopita - Mei 12, 2023 anatarajiwa kusikwa kesho kijijini mwake Rondo, Lindi. (Picha na Ikulu).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko1@protonmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



Baada ya Vita Kuu ya Kwanza, 1918, Ujerumani, Japan, Korea Kusini, Singapore na hata Malaysia zilikuwa zikipokea misaada kutoka Marekani na Uingereza, ilipotimia miaka 20 baadaye, nchi hizo zote zilikuwa sikitoa misaada, ajabu nchi za Afrika, baada ya miaka 60 ya uhuru, bado zinapanga namna ya kupokea misaada kutoka Ulaya na Marekani. Ajabu sana, zamani lawama kwa umasikini kwa Afrika ilitupwa kwa wakoloni, sasa leo sijui nini kilaumwe - Ali Mufuruki (marehemu) alikuwa mfunyabiashara kutoka Tanzania

Habari

Miradi ya PPP kuifungua nchi

Na Mwandishi WETU

TANZANIA inatarajia kuingia kwenye ramani ya nchi ambazo zimefanikiwa zaidi kiuchumi kwa kutumia mifumo ya kujenga na kuendesha miundombinu ya kisasa kwa ushirika na sekta binafsi.

Sambamba na hatua hiyo, serikali pia imedhamiria kwamba miradi mingi mikubwa ya kiuchumi na kijamii itaanza kutekelezwa hivi karibuni kupitia utaratibu wa ushirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi yaani PPP (Public Private Partnership).

Kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa miradi hiyo utagharamiwa na sekta binafsi na kuiwezesha serikali kutumia fedha zake katika miradi mingine hasa ya huduma za kijamii.

Haya yamebainishwa na Kamishna wa PPP, David Kafulila, katika mahojiano na gazeti hili, Pambazuko.

Katika mahojiano hayo maalum, Kafulila alisema miradi mingi itakayotekelezwa chini ya mfumo wa PPP itahusisha ujenzi wa miundombinu, hasa barabara hali kadhalika uzalishaji na usambazaji wa umeme.

“Hii inamaanisha kuwa sasa serikali itaweza kutumia fedha zake katika maeneo mengine ya huduma za jamii, kwani miradi hii itagharamiwa kwa kiasi kikubwa na sekta binafsi.

“Lakini pia miundombinu kama barabara na uzalishaji wa umeme ni moja ya miradi wezeshi katika ujenzi wa uchumi, hivyo tutakuwa katika nafasi nzuri zaidi ya kuimarisha uchumi chini ya utaratibu huu,” alisema Kafulila ambaye ni mbunge wa zamani wa Kigoma Kusini.

Kafulila alisema ujenzi wa barabara kadhaa, ikiwamo ya Kibaha – Chalinze – Morogoro, Isongole – Tunduma na zile za ndani ya Jiji la Dar es Salaam, zinatarajiwa kufungua njia za usafiri na kuwezesha usafishaji wa mizigo na abiria kwa haraka.



Rais Samia Suluhu Hassan sasa anaifungua nchi.

“Moja kati ya mambo yanayokwamisha uchumi ni njia hafifu za usafiri na usafishaji. Kwa mfano; Tunduma ndiyo kituo cha mpakani kikubwa kuliko vyote nchini kwani kinahudumia takribani asilimia 70 ya mizigo yote inayoingia kupitia Bandari ya Dar es Salaam...

... Hii inakifanya kipande cha barabara kati ya Isongole pale Mbeya na Tunduma kuwa chenye msongamano mkubwa wa magari na iwapo njia hii itapanuliwa tutarahisisha usafirishaji wa mizigo inayokwenda nchi jirani,” alifanua.

Aliutaja mradi ambao utekelezaji wake unatarajiwa kuanza mapema kuwa ni ujenzi wa barabara ya njia nne kati ya Kibaha na Chalinze ikiwa ni sehemu ya mradi wa ujenzi wa barabara ya kilometa 205 kati ya Kibaha na Morogoro.

Kafulila alisema tayari andiko la mradi wa kipande cha Barabara ya Kibaha – Chalinze limeshaandaliwa na Kampuni ya Chiel kutoka Korea ambayo ililipya dola milioni 7.1 kwa ajili ya kazi hiyo.

Ujenzi wa kipande hicho unatarajiwa kugharimu dola milioni 350 na kipande cha Chalinze – Morogoro kitagharimu

Chozi la Kikwete kumlilia Membe



Rais Kikwete akiwa na Membe

Na Jakaya KIKWETE

NIMEPOKEA kwa mshituko na huzuni kubwa taarifa ya kifo cha Mheshimiwa Bernard Kamilius Membe, NImemfahamu miaka mingi, tumetoka naye mbali na tumesaidiana kwa mengi. Familia zetu, na mapito ya maisha yetu yamehusiana sana.

Bernard Kamilius Membe alikuwa mtu wa msaada mkubwa kwangu katika maisha yangu ya kikazi na kisiasa. Nilimuamini na kumtumainia katika nafasi zote alizohudumu kwenye baraza langu la mawaziri. Aliwahi kuwa Naibu Waziri katika Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Nishati na Madini.

Halikadhalika, aliwahi kuwa waziri wangu wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa miaka tisa, ambapo alifanya kazi kubwa na nzuri ya kuendeleza maslahi ya Tanzania katika medani za kimataifa.

Nautambua mchango wake mkubwa alioutoa kwenye Chama Cha Mapinduzi (CCM) alipokuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa, Mjumbe wa Kamati Kuu na Katibu wa Siasa na Uhusiano wa Kimataifa katika Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa. Katika nafasi zote hizo, alijitoa kwa moyo wake wote na kuacha alama za kudumu.

Nilimfahamu Mheshimiwa Membe

kama mwanadiplomasia mboenzi, mwanaharakati makini, msomi mzuri, mcha Mungu, mzalendo, mchapakazi hodari na mtu jasiri ambaye hakuogopa kusema na kulisimamia analoliamini. Hakika taifa limepoteza mmoja wa watu wake muhimu.

Natoa salaam za rambirambi na mkono wa pole kwako shemeji yangu Dorcas Membe na watoto wenu Cecilia, Richard na Dennis, pamoja na wajukuu, ndugu na jamaa wa marehemu Bernard Kamilius Membe.

Nawapeni pole kwa msiba mkubwa uliowakuta, lakini napenda kuwahakikishia kuwa hamko wapweke. Mimi pamoja na mke wangu Salma na wana familia wetu wote, tuko pamoja nanyi katika majonzi na kuomboleza.

Tunawaombea kwa Mola awajalie moyo wa subira na ustahamilivu katika kipindi hiki kigumu mnachopitia.

Tukumbuke daima, "sisi sote ni waja Wake, na kwake tutarejea." Bwana ametoa, Bwana ametwaa, jina lake lihimidiwe.

Tumuombee kwa Mola marehemu mpendwa wetu, apumzike kwa amani na roho yake aiweke mahala Pema Peponi.

Amina.

Mwandishi wa makala haya ya Tanzania ni Rais (mstaafu) wa Tanzania, akimwandikia mke wa Bernard Membe, Dorcas.

Habari

TTB kutumia michezo kupaisha utalii

Na Scovya MANASE

TANZANIA imedhamiria kuendelea kutangaza vivutio vya utalii nje ya nchi hiyo kwa kutumia michezo.

Tayari Bodi ya Utalii ya Tanzania (TTB) kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii, imeanza “mbio” za kuhakikisha hilo linafanikiwa kwa kuingia makubaliano ya kimkataba na baadhi ya timu za michezo vya Marekani

Mkataba wa utekekezaji wa makubaliano haya ulifungwa wiki iliyopita katika uwanja wa Lumen, ulioko Jiji la Seattle, Marekani baina ya Serikali ya Tanzania na Kampuni ya Vulcan, inayosimamia baadhi ya timu za soka na mpira wa kikapu (basketiboli).

Timu zitakazohusika kwenye mkataba huu ni pamoja na timu za soka za Seattle Sounders, Seattle Seahawks na Portland Trailblazers inayoshiriki Ligi Kuu ya Mpira wa Kikapu (NBA).

Kampuni ya Vulcan inayojihusisha na biashara ya majengo, ardhini na ushauri wa kibiasara, inamilikiwa na mwazilishi mwenza wa kampuni Tajiri ya Microsoft; wabunifu wa mifumo ya kompyuta.

Akiwa nchini Marekani mwishoni mwa wiki, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii wa Tanzania, Dkt. Hassan Abbas alisema serikali imedhamiria kuweka nguvu kubwa kukuza sekta

ya utalii kwa kupitia njia mbalimbali, ikiwamo kushirikisha timu za michezo maarufu, ikiwamo soka, mpira wa kikapu na pia michezo mingine.

“Lengo letu ni kuhakikisha vivutio vya utalii Tanzania vinawafikia watalii wengi Zaidi ili wavutike kuja kufanya shughuli mbalimbali za utalii, hii itasadia kuongeza mapato ya serikali na kusukuma mbele maendeleo ya nchi na watu wake,” alisema Dkt. Abbas.

Dkt. Abbas aliambatana na Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) Damas Mfugale ambaye bdi yake ndiyo yenye jukumu kubwa la kuongoza kutangaza vivutio vya utalii.

Miliki wa timu hizo za michezo ambazo zimeingia mkataba na Tanzania, Adrian Hanauer alisema ni jambo la furaha kusaini mikataba hiyo na kuwataka wafanyabiashara wa Marekani ambao hawajawahi kutembelea Tanzania, kupanga kufika ili kuona vivutio vingi vya utalii.

Hanauer ambaye aliwahi kutembelea baadhi ya vivutio vya Tanzania, ikiwamo kutazama wanyama katika maeneo ya utalii ya Ngorongoro na Serengeti alihimiza “watu wote ambao hawajafika Tanzania, kujipanga kufika kwa ajili ya kushuhudia namna dunia inavyopendeza kupitia Tanzania.”



Mkurugenzi Mkuu wa TTB, Damas Mfugale (kushoto) akiwa pamoja na ofisa kutoka Kampuni ya Vulcan. Kulia ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dkt. Hassan Abbas.

Madaktari ‘wafura’ mwenzao kuuawa

Na Tryruckias MFINANGA

KIFO cha daktari mfawidhi ya Wilaya Kya Tarime, Mara, Isack Daniel Athuman kilichotokea Mei 3, 2023 – kwa kukatwa mapanga, kimewaibua madaktari wenzake wakitaka kupatikana kwa wauaji haraka.

Madaktari hao wameonyesha hasira zao wakati wakizungumza na Pambazuko na wengine kupitia kurasa zao za mitandao ya kijamii, huku wakilaani kitendo hicho kwa kukiita cha “kikatili na unyama uliopitiliza.”

Dkt. Isack aliyekuwa akitumika katika Kituo cha Afya cha Kerende - Nyangoto, Kata ya Nyamongo, aliuaa na wale wanaoitwa “watu wasiojulikana” usiku wakati akirejea nyumbani kwake kutoka kazini. Wauaji hao baada ya kuuu, walichukua pikipii yake na kutokomea.

Rais mstaafu wa Chama cha Madaktari Tanzania, Elisha Osati akizungumzia kifo hicho amesema – “Haikubaliki, Dkt. Isack ni mmoja wa Madaktari 1000 tuliopewa na Rais John Magufuli katika maadhimisho ya Siku ya Madaktari 2020, huyu alikuwa tayari kuwahudumia wananchi vijijini, tena bila kulazimishwa na akaenda kufanya kazi huko, alikuwa mzalendo wa kweli,” amesema Dkt. Osati.

Dkt. Osati ameitaka serikali kwa kutumia vyombo vyake vya usalama na dola kuhakikisha wahusika wote wa kifo cha Dkt Isack wanakamatwa, kufikishwa kwenye vyombo vya sheria na haki kutendeka.

“Ni ujinga wa kiwango kikubwa sana watu kuuu daktari ambaye amekuwa akiwatuibu na kuwaepusha vifo, kusaidia wakinamama kujifungua salama, kufanya upasuaji, leo watu haohao wanamuaa! Inasikitisha sana, ni heri sasa, serikali isipeleke madaktari huko hadi kila aliyehusika akamatwe na mtandao wa wauaji kuwekwa wazi.” Analaani Dkt. Joshua Jeremia kupitia mtabdao wa Twitter.

Ngw’ina Iseme, daktari kutoka



Dkt. Isack Athuman

Mbeya anasema – “serikali itoe tamko kwamba inawasaka wauaji na iwapate na wachukuliwe hataa kali” na anaongeza – “wafanyakazi wa idara ya afya tunafanya kazi kwenye mazingira magumu sana. Tulisoma kwa taabu na bado tunaishi kwenye mazingira ya shida mno. Matukio ya kuuawa yatafanya watumishi wa afya kukata tamaa kufanya kazi kwenye maeneo fulani hapa nchini.”

Mwananchi mmoja anayejitambulisha kuwa daktari katika mtandao wa Twitter (@RockfellaElish2) anasema – “nadhani ni wakati sasa wa kuviwezesha vituo vya afya kuwa na gari au magari ya kutosha na bajeti kwa ajili ya mafuta, ili yatumike kupeleka kazini na kurudisha madaktari nyumbani ili kuepusha vifo vya namna hii, kifo cha Dkt. Isack, Pamoja na kusikitisha, lakini kiqe chachu kuhakikisha serikali iatenga bajeti kwa ajili ya usafiri kwa watoa huduma za afya.”

Waziri wa Afya, Ummu Mwalimu ametoa pole kwa madaktari na waudumu wa fya na kwamba analaani kitendo hicho na kueleza kusikitishwa kwake na kuomba vyombo vya dola kufanya kila linalowezekana kukamatwa kwa wahusika hao na kufikishwa kwenye vyombo vya haki.

Tanzia

‘Moyo wangu wavuja damu’

Na **Abdulkarim MALISA**

WIKI iliyopita nilikuwa kwenye majukumu yangu ya kawaida nje ya kituo changu cha kazi – nilikuwa maeneo ya Kanda ya Ziwa Victoria.

Ukanipigia simu na kunihimiza kwamba nisiondoke kurejea Dar es Salaam, bila kufika Tarime, nione unapofanya kazi, maana tangu upangwe huko sijawahi kufika.

Jumanne iliyopita nikatoka Geita kwenda Chato. Jumatano nikaanza safari kutoka Chato kwenda Mwanza. Nikakupigia kuwa nitalala Mwanza ili siku inayofuata, Alhamisi nimalizie safari ya kuja huko kazini kwako. Ukapokea taarifa hiyo kwa furaha kubwa.

Nikakutania kwamba upo Mkoa wa Mara, inabidi uwe imara. Nikakukumbusha enzi za shule ya msingi ambako kila ukionewa unakuja kunishitakia, nami naenda kuwapa “haki ya kikatiba wale waliokuonea.”

Baada ya kumaliza elimu ya msingi, ulipangwa kwenda kuendelea na masomo huko Shule ya Sekondari Ifunda, nilikushauri usimuonee mtu, lakini ujifunze kujitetea. Ukaniambia kuwa sasa hivi huonewi tena, maana umeanza kupata kitambi.

Wakati ule walikuonea sana kwa kuwa hukuwa na mwili. Tukacheka na kuagana tukitarajia kuonana kesho yake.

Nikaingia Mwanza usiku. Nikakupigia simu hukupokea, nikakuandikia ujumbe wa simu (sms) kuwa nimefika Mwanza na kesho nitakuwa Nyamongo, Tarime.

Alhamisi nikaamka mapema – muda wa saa moja. Nikakuta miito mingi; 32 ambayo haikupokelewa (missed calls) kutoka kwa ndugu wa karibu, hii ilisababishwa na kutoa sauti ya miito ili niweze kupumzika, hivyo sikusikia ikiita.

Hata hivyo, baada ya kuamka na

kushika simu, nilishtuka kubaini kuwa watu wengi wa karibu Zaidi, hata ambao hatuna kawaida ya kuwasiliana kwa simu, wamenipigia.

Nikaona miito ya simu ya mama na ndugu wengine ambayo haikupokelewa. Kabla sijawapigia nikasoma kwanza ujumbe was imu... ohhh Mungu wangu - nilijihisi nipo ndotoni. Eti umefariki? Nikasema haiwezekani, maana jana tumewasiliana na hata hii safari yanguni ya kuja kwakia.

Mdogo wangu kwanini wamekufanyia ukatili huu? Uliwakosea nini? Mbona hujawahi kuwa na shida na mtu? Kwanini hawakusubiri hata nifike kwanza? Ngingekutetea kama ilivyokuwa shule ya msingi.

Singekubali kuina damu yako inamwagika mbele yangu, labda watuue wote. Ule usiku nilipokupigia simu hukupokea kumbe ulikuwa unapigania roho yako katikati ya “mbwa mwitu wakali?”

Safari yangu ya Tarime ikaishia Mwanza.

Badala ya wewe kunipokea Tarime, mimi ndiyo napokea mwili wako hapa Mwanza, tena ukiwa huna pumzi. Eti wamekuua kwa kukukata mapanga jamani!

Namuwaza mkeo na mwanao. Hawa walikuhitaji zaidi kuliko watu wengine. Lakini umewaacha mapema mno. Mkeo amebaki mjane kabla hata ndoa yenu haijafikisha mwaka mmoja.

Mwanao amebaki yatima akiwa bado kichanga. Kwaheri mdogo wangu Isack.

Mungu atatukutanisha tena huko mbele ya safari, ambako naamini hakuna tena atakayekuonea.

Acha moyo wangu uvuje damu kwa sasa.

Lala salama Dkt. Isack wetu.

• **Mwandishi ni kaka wa marehemu Dkt. Isack Daniel**

Mfumo mpya wa elimu waja

Na Mwandishi WETU

TAYARI Serikali ya Tanzania iko mbioni kubadilisha sera na mfumo wa elimu. Je, muundo wa mfumo mpya wa elimu ukoje?

Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, inapendekeza muda wa miaka sita kwa ajili ya elimu ya msingi ili kukidhi matakwa ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 - Toleo la Mwaka 2023. Aidha, serikali inapendekeza umri wa kuanza Darasa la Kwanza uwe miaka sita.

Pambazuko limeona mfumo huo mpya waelimu na kwamba kulingana na matakwa ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023, Elimu ya Msingi inapaswa kutanguliwa na mwaka mmoja wa Elimu ya Awali kwa watoto wenye umri wa miaka mitano.

Vilevile, serikali inapendekeza muda wa Elimu ya Sekondari uendelee kuwa miaka sita; yaani minne ya Sekondari Hatua ya Chini na miwili ya Sekondari Hatua ya Juu.

Mapendekezo haya yamezingatia maoni ya wadau pamoja na uzoefu kutoka nchi mbalimbali.

Kama inavyoelekezwa na Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023, serikali inapendekeza kwamba elimu ya lazima itolewe kwa muda wa miaka kumi.

Yaani, miaka sita ya Elimu ya Msingi na miaka minne ya Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini.

Hii ina maana kwamba kila mwanafunzi atakayeanza Darasa la Kwanza ataendelea kubaki shuleni hadi Kidato cha Nne.

Kwa sababu hiyo, hakutakuwa na mtihani wa kuhitimu Elimu ya Msingi. Badala yake kutakuwa na upimaji wa kitaifa wa Darasa la Sita kama ilivyo sasa kwa wanafunzi wa Darasa la Nne na Kidato cha Pili.

Ili kukidhi maoni ya wadau juu ya umuhimu wa kuwapatia wahitimu wa elimu ya lazima stadi zitakazowawezesha



Waziri wa Elimu Prof. Adolf Mkenda

kushiriki katika ulimwengu wa kazi, serikali inapendekeza kunyumbulisha Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini katika mikondo miwili. Yaani Mkondo wa Elimu ya Jumla na Mkondo wa Elimu ya Amali (Ufundi).

Kila shule ya sekondari ya chini italazimika kuwa na mkondo wa Elimu ya Jumla na mkondo wa Elimu ya Amali.

Mwanafunzi atachagua mkondo kulingana na matakwa, uwezo na malengo yake ya maisha.

Mwanafunzi atakayepitia mkondo wa Elimu ya Amali atakuwa na uwezo wa kuajiriwa au kujajiri mara baada ya kuhitimu Kidato cha Nne.

Mkondo wa Elimu ya Amali utagawanyika katika michepuo ya fani mbalimbali kama kilimo, ufugaji, umakenika, biashara, ufugaji wa nyuki, uchimbaji madini, na urembo.

Wahitimu wa mkondo wa Elimu ya Amali watafanya mtihani ya aina mbili na kupewa vyeti viwili. Kuna cheti cha kuhitimu elimu ya sekondari na cheti cha Elimu ya Amali.

Habari**Miradi ya PPP kuifungua nchi***Inatoka Uk. 4*

dola milioni 510.

Alisema kampuni 13 tayari zimeomba utekelezaji wa ujenzi wa Barabara ya Kibaha – Chalinze na hatua iliyopo sasa ni kufanya uchambuzi ili kupipata kampuni tatu zitakazoshindanishwa ili kuipata kampuni itakayopewa kazi hiyo.

Pia kuna mpango wa ujenzi wa barabara za ndani na kuzunguka Jiji la Dar es Salaam ambazo taftiti zinaonyesha kuwa zimekuwa na mzunguko wa chini katika usafirishaji kutokana na ufinyu na ubovu wa miundominu.

“Ili kuifungua Dar es Salaam, kuna miradi ya ujenzi wa barabara za ndani na kuzunguka jiji. Pia kuna mpango wa kupanua mtandao wa barabara za mabasi ya mwendo kasi - BRT (Bus Rapid Transit) na pia ujenzi wa treni za abiria ndani ya jiji,” alisema Kafulila.

Miradi ya umeme

Kafulila alisema pia kuna miradi kadhaa ya uzalishaji na usambazaji wa umeme ambayo itatekelezwa kupitia mpango wa PPP na kuiwezesha nchi kujiamarisha katika eneo hilo.

Alisema moja ya miradi hiyo ni uzalishaji wa umeme kwa kutumia joto ardhi katika eneo la Ziwa Ngozi mkoani Songwe.

“Huu ni mradi ambao andiko lake litakapokamilika, tunatarajia kupata mwekezaji haraka kwa sababu hivi sasa kuna kampuni nyingi huko nje ambazo zinatafuta fursa ya kutekeleza miradi kama hii,” alifafanua.

Aidha, alisema kuna mpango wa ujenzi wa miradi ya uzalishaji umeme kutokana na upepo katika maeneo ya mikoa ya Kilimnairo, Dodoma na Singida. Alisema kwa ujumla miradi hiyo itazalisha megawati 210 za umeme.

Kafulila alisema kwa mara ya kwanza nchi itatekeleza mradi wa usambazaji wa umeme kupitia kampuni binafsi kupitia

mradi wa kuunganisha umeme kati ya Tanzania na Malawi.

“Kwa kawaida, kazi ya kusambaza umeme imekuwa ikifanywa na Tanesco. Mradi huu unaohusisha ujenzi wa njia ya umeme yenye umbali wa kikometa 82 utakuwa wa kwanza kwa kampuni binafsi kushiriki katika kusambaza umeme nchini,” alisema.

Shilingi trilioni 21

Kafulila amesema kuwa jumla ya miradi 29 inatarajiwa kutekelezwa nchini kupitia mpango wa PPP na miradi 14 tayari imeshafanyiwa upembuzi yakinifu.

Utekelezaji wa miradi hiyo unatarajiwa kugharibu dola bilioni 9 za Marekani au Sh21.2 trilioni, kiasi ambacho ni kikubwa cha fedha kwa vipimo vya uchumi wa Tanzania hivi sasa.

“Kwa maana nyingine, kama isingekuwa kwa PPP, serikali ingelazimika kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hii. Lakini, chini wa mpango huu, serikali itapata nafuu kwa sababu fedha ambazo ingepaswa kuzielekeza kwenye miradi hii, itazipeleka kwenye mambo mengine kama vile kuimarisha huduma za jamii,” anasema Kafulila.

Mbunge huyo wa zamani alibainisha kuwa jambo la kufurahisha kuwa taftiti unaonyesha Watanzania wapo tayari kuipokea na kuitumia miradi ya aina hiyo ambayo baadhi yake itahusisha utozaji wa tozo kwa watumiaji.

“Katika kila mradi tunaoufikiria, kwenye utafiti wa awali huwa tunapima kiasi cha kukubalika kwa mradi husika miongoni mwa Watanzania na matokeo yanaonyesha kuwa wananchi wengi wanaikubali miradi hii...”

... Kwa mfano watumiaji wa Barabara ya Morogoro au Isongole - Tunduma, wengi wapo tayari kutumia barabara ya kulipia ili kukwepa foleni ambayo inawachelewesha kuwahi kwenye shughuli zao,” ameongeza Kafulila.

Balile Makamu wa Rais EAES

Na Mwandishi WETU

MWENYEKITI wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile amechaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jumuiya ya Wahariri Afrika Mashariki (EAES) kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Balile alichaguliwa kwa kura zote kutoka kwa viongozi wakuu wa majukwa ya wahariri kutoka nchi wanachama wa EAES, ambazo ni Kenya, Uganda, Ethiopia na Tanzania.

Katika uchaguzi huo, Daniel Kalinaki wa Jukwaa la Wahariri Uganda aliukwaa urais wa EAES.

Katiba ya EAES inaeleza kuwa rais na makamu wake, wataongoza kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Mei 12, 2023 hadi Mei 11, 2024. Baada ya hapo, Balile atakuwa Rais EAES moja kwa moja;



Deodatus Balile

kuanzia Mei, 2024 hadi Mei, 2025.

Katiba ya EAES inatoa nafasi ya kumwanda kiongozi wake ajaye kwa mwaka mmoja baada ya kumchagua kama sehemu ya maandalizi ya kuifahamu vyema kazi yake kabla ya kushika madaraka hayo rasmi.

Siku yangu ikifika

1. Dongo laungoja mwili,
siku hiyo ikifika,
Ni tarehe ishinambili,
au saba bila shaka,
Ni Tumbi hosipitali,
Kawogo sina hakika,
**Siku yangu ikifika,
kwenye vumbi nitalala.**

2. Kwenye vumbi nitafika,
kifusi unisubiri,
Sintoweza kutoroka,
sifanyi mie kiburi,
Siku hiyo ikifika,
unifunike kwaheri,
**Siku yangu ikifika,
kwenye vumbi nitalala.**

3. Roho itaacha mwili,
siku sijaikariri,
Ni homa au ajali,
sababu sitabiri,
Ni siri yake jalali,
'aka' mimi sibashiri,
Siku yangu ikifika,

kwenye vumbi nitalala.
4. Nikakeshe Kanisani,
roho yangu itatoka,
Nishinde msikitini,
ziraeli atafika,
Au niwe mpagani,
mauti yatanifika,
**Siku yangu ikifika,
kwenye vumbi nitalala.**

5. Nikaishi Marekani,
kwenye nyumba za kitishi,
Nikakae uhindini,
kwenye sifa ya marashi,
Raha ya muda fulani,
milele siwezi ishi ,
**Siku yangu ikifika,
kwenye vumbi nitalala.**

6. Kwenye vumbi nitarudi,
hilo nalijua fika,
Nitamuacha waridi,
machochi yakimtoka,
Maisha hatofaidi,

mumewe nimetoweka,
**Siku yangu ikifika,
kwenye vumbi nitalala.**

7. Kifo hakina simle,
Kawogo hilo nawapa,
Si fimbo za tokomile,
na kuwa utazikwepa,
Ni mtego wa tetele,
mwindaji hatoki kappu,
**Siku yangu ikifika,
kwenye vumbi nitalala.**

8. Hapa ni mwisho wangu,
kaditama ni tamati,
Ninaomba walimwengu,
tutafakari mauti,
Tuzidi kuomba Mungu,
hakika tuisaliti,
**Siku yangu ikifika,
kwenye vumbi nitalala.**

**Al- Watan,
Albert Kawogo
(mwanamosi) Bagamoyo.**

Mtazamo Wangu

Nani ataiponya DR Congo?

Na Mwandishi MAALUM

BAADA ya jeshi la serikali kushindwa kukabiliana na waasi, Umoja wa Mataifa (UN) ukaamua kupeleka kikosi cha wanajeshi (Monusco) ili kuhakikisha amani inapatikana katika Nchi ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).

Lakini, baada ya miaka kadhaa ikabainika kuwa hata hilo jeshi lililopelekwa na UN, halijafanikiwa kutekeleza kikamilifu jukumu ambalo lilipewa.

Hapo, nchi jirani, chini ya mwamvuli wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), wakaamua nao kujitosa katika harakati za kusaka amani nchini DRC kwa kupeleka wanajeshi wake nchini humo, hasa katika eneo la mashariki.

Vikosi hivyo vya EAC, vikianza na wanajeshi kutoka Kenya, vilivasili nchini humo mwishoni mwa mwaka jana. Baadaye wanajeshi kutoka Burundi nao wakapelekwa.

Lakini, katika hatua ambayo haikuwashangaza baadhi ya watu na kuwashangaza wengine kadhaa, taarifa zinaonyesha kuwa hata hilo jeshi lililopelekwa na EAC, nalo ni kama limeshindwa kuifanya kazi hiyo ipasavyo.

Hivi sasa, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) inapanga kupeleka vikosi kusaidia kuleta amani mashariki mwa Congo.

Mlolongo huu wa matukio yanayoambatana na jitihada za kuisaidi DRC kupata amani, unaonyesha jinsi ugumu uliopo kulifikia lengo hilo.

Tatizo kubwa katika hili ni kuwa hakuna anayekuja na sababu nzito na za msingi kuonyesha kuwa kwa nini kila hatua inayochukuliwa inashindwa.

Ndio maana hadi hii leo, bado ufumbuzi wa migogoro wa kivita mashariki wa DRC imeendelea kuwa mfupa mgumu. Kwa kawaida ni vigumu sana kupata ufumbuzi wa tatizo ambalo hujui chanzo kikubwa cha tatizo hilo.

Inafahamika kwa ujumla tu kuwa



Rais Tshisekedi

utajiri mkubwa wa rasilimali uliopo katika eneo hilo la mashariki mwa DRC, ndio kiini cha kudumu kwa migogoro na mapigano yanayoendelea.

Uamuzi wa kupeleka jeshi la EAC ulifikia baada ya lawama za muda mrefu kwa wanachama wa jumuiya hiyo kuamua kutofumbia macho na kuacha mwanachama mwenzao akiteseka kwa mapigano kwa miaka kadhaa huku wao wakikaa na kuangalia tu.

Nchi hizo ziliamua kuchukua hatua baada ya DRC kujiunga na jumuiya hiyo.

Ingawa awali ilionekana kuwa mpango huo ni mzuri na muafaka kwa sababu nchi zinazoathirika na mgogoro huo ndizo ziliamua kuushughulikia, watu wengi wakaamini kuwa utatuzi wa kudumu sasa utapatikana.

Lakini, katika kipindi kifupi kisichofikia hata mwaka mmoja, imebainika kasoro nyingi na kubwa katika mpango huo wa kuisaidia DRC kuleta amani nchini humo.

Rais wa DRC, Felix Tshisekedi amenukuliwa akisema kuwa halitaki jeshi la EAC nchini mwake. Amefikia hatua ya kutoa muda hadi mwezi Juni, yaani mwezi ujao, jeshi hilo liwe limeondoka.

Hilo likitokea, itakuwa jeshi la EAC limefanya kazi kwa kipindi cha chini ya mwaka mmoja!

Tshisekedi analituhumu jeshi hilo la

Nani ataiponya DR Congo?

Inatoka Uk. 12

kikanda kwa kushikamana na waasi na kuacha kutekeleza majukumu yake ya msingi.

Alibainisha hayo wakati akizungumza alipokuwa ziarani huko Botswana baada ya kutoka kwenye kikao cha dharura cha SADC kilichoamua kupeleka jeshi lake huko DRC.

Tshisekedi anasema jeshi la EAC limekuwa mshirika wa kundi la M23, ambalo ndilo kundi kubwa la waasi ambalo limekuwa likiyumbisha amani ya eneo la mashariki mwa DRC kwa miaka kadhaa sasa.

Kauli hii ya Rais wa DRC inakuja siku chache tu baada ya aliyekuwa kamanda wa Jeshi la EAC huko DRC, Meja Jenerali Jeff Nyagah kutoka Kenya, kuamua kuachia nafasi hiyo na kurejea nyumbani.

Meja Jenerali Nyagah anasema ameamua kuachia ngazi na kuondoka DRC kutokana na sababu kadhaa ikiwamo tishio dhidi ya maisha yake.

Kwa upande mwingine, EAC imetetea utendaji wa jeshi lake mashariki mwa DRC ikisema kuwa limekuwa likitekeleza majukumu yake ipasavyo na tangu liingie nchini huko limepata mafanikio kadhaa.

Labda Tshisekedi anajivunia jeshi jipya la SADC litakalopeleka nchini mwake. Lakini akumbuke kuwa hilo halitakuwa jeshi la kwanza kuingia DRC kwa lengo la kutuliza mapigano.

Kwa kuwa ilidhaniwa kuwa kuingia kwa EAC kutasaidia kutuliza mapigano, bado ni vigumu kuhakikisha kuwa hata jeshi la SADC litasaidia kwa kiasi kikubwa.

Mapigano haya ya mashariki mwa DRC yameifanya nchi hiyo kukosana na mataifa mengi. Juzi, dunia ilishuhudia jinsi DRC ilivyokuwa ikijibishana kibabe na Rwanda kiasi cha kufikia kutishiana kutumia nguvu za kijeshi dhidi ya mwingine.

Sasa Tshisekedi anagombana na majirani zake wote wa EAC, hivi anadhani ni nani hasa anaweza kumsaidia



Rais wa Rwanda Paul Kagame

kupambana na tatizo linalomkabili?

Kwa watu wanaofahamu diplomasia, walipomsikia Tshisekedi akiliponda jeshi la EAC hadharani, walipatwa na mshituko mkubwa hasa ukizingia uzito wa tatizo ambalo jeshi hilo lilikwenda kukabiliana nalo.

Kama Tshisekedi ameshindwa kuelewana na Monusco, ameshindwa kuelewana na jirani yake Rwanda, ameshindwa kuelewana na washirika wenzake wa EAC, hivi ni nini kampa imani kuwa ataweza kuelewana na SADC?

Tshisekedi na DRC wanapaswa kulipa suala hilo fikra kali. Anapaswa kujiuliza ni kwa nini mgogoro huu umedumu kwa muda mrefu namna hii?

Atabaini kuwa hao wote anaogombana nao na kuwaona hawamsaidii katika kutatua matatizo nchini mwake wala siyo sehemu ya chanzo au chanzo cha mgogoro unaomkabili.

Asipoangalia, Tshisekedi anaweza kugombana na majirani zake wote ambao wanajitolea kumsaidia na hapo atakuwa akichochea moto wa kuongezeka kwa mapigano kwa kuwa wote wanaweza kumsusa.

Ikifika mahali kila mtu akamchoka, Tshisekedi atajikuta amebakia peke yake, huku akiwa anakabiliwa na uasi mkubwa kuliko huu anaokabiliana nao hivi sasa.

Kumbukumbu

Kwanini Barabara ya Shekilango?

Na Mzee wa ATIKALI

BARABARA ya Shekilango ni moja kwa njia maarufu katika Jiji la Dar es Salaam, Tanzania kutokana kuwa kiungo cha barabara za Morogoro na Ali Hassan Mwinyi.

Shekilango ni barabara yenye urefu unaoelezwa kufikia kilometa 3.7, upana wa mita 22, ikiwa na njia nne za magari, njia za watembea kwa miguu, taa za kuongoza vyombo vya moto na waenda kwa miguu.

Hata hivyo, pamoja na kubeba umaarufu mkubwa, watu wengi hawana taarifa sahihi kwa nini ilipewa jina la Shekilango.

Barabara hiyo ilipewa jina la Shekilango, ikiwa ni kuweka kumbukumbu ya Mtanzania aliyetitwa Hussein Ramadhani Shekilango. Huyu aliwahi kuwa waziri na Mbunge wa Korogwe.

Shekilango aliingia mara ya kwanza bungeni baada ya kushinda kwenye uchaguzi mkuu uliofanyika Jumapili, Oktoba 26, 1975 ambapo alipata kura 34, 845 huku mpinzani wake, Athumani Mhina akiambulia kura 14, 224.

Novemba 9, 1975, Rais Julius Nyerere alimteua Shekilango kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Utawala) akiwa chini ya Makamu wa Pili wa Rais na Waziri Mkuu, Rashid Mfaume Kawawa.

Mwaka 1977, yalifanyika mabadiliko makubwa kwenye Baraza la Mawaziri ambapo aliyekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Edward Moringe Sokoine aliteuliwa kuwa Waziri Mkuu akichukua nafasi ya Kawawa. Katika mabadiliko hayo, Shekilango akabakizwa kwenye nafasi yake, lakini chini ya uongozi wa Sokoine.

Kabla ya kuwa mbunge, Shekilango alikuwa Meneja Mkuu wa Shirika la Usagaji la Taifa lililoanzishwa mwaka 1968 na Sheria ya "The National Milling Corporation Act, 1968".

Vita vya Kagera vyarindima



Shekilango

Mwishoni mwa mwezi Novemba 1978, majeshi ya Uganda yalivamia nchi sehemu ya ardhi ya Tanzania na kusababisha kuanza kurindima baada ya njia za kutatua mgogoro huo kidiplomasia kushindikana.

Sokoine na Shekilango walikuwa ni miongoni mwa viongozi walioshiriki kikamilifu kufuatilia kwa karibu zaidi usimamizi wa uongozi wa serikali ya Uganda baada ya Tanzania kuibuka washindi na kumseta Idd Amini nje ya Uganda.

Viongozi hawa walitumwa na Rais Nyerere (sasa marehemu) – kwa kushirikiana na baadhi ya viongozi wa serikali ya mpito ya Uganda baada ya Idd Amini kukimbia nchi yake na waiukuwa na kazi ya kupeleka taarifa kwa Rais Nyerere.

Shikilango apanga kumuona Nyerere

Jumapili, Mei 11, 1980, Shekilango alikuwa na miadi ya kukutana na Rais Nyerere mjini Arusha kwa ajili ya mazungumzo na kumpa taarifa za kilichokuwa kikiendelea Uganda.

Asubuhi ya Jumapili hiyo, Shekilango aliongoza msafara wa baadhi ya Watanzania wengine – wakiwamo wanajeshi waliokuwa bado Uganda

Kwanini Barabara ya Shekilango?

Inatoka Uk. 14

kwenda kukutana na Rais Nyerere, hivyo “walikwea” ndege ndogo kwenye Uwanja wa Entebbe na kuanza safari ya kutua Arusha.

Ndege waliyotumia ilikuwa ni aina ya Casena 402 yenye uwezo wa kubeba abiria wanane. Walioukwamo ndani ni Shekilango mwenyewe, Balozi wa Tanzania nchini Uganda, Faraji Kilumanga, mwanadiplomasia Idd Msechu, Luteni Peter Mallya, Luteni Luoga, koplo Petro Magunda na private Stephen Mtawa.

Hata hivyo, ndege hiyo haikuweza kufika uwanja wa Arusha salama, ilipata ajali ikiwa imeingia anga la Arusha na kwamba abiria wote walikuwa ndani yake walifariki dunia.

Shekilango azikwa kishujaa

Shekilango aliyekuwa kipenzi cha wana- Korogwe, alizikwa Kijiji cha Jitengeni, Mombo, Korogwe, mkoani Tanga. Mazishi hayo yalihudhuriwa na umati mkubwa wa watu ulioweka rekodi ya aina yake wilayani Korogwe.

Katika kumuenzi, shule moja huko Mombo ikapewa jina lake; Shule ya Sekondari Shekilango, huku wilayani Kinondoni, Dar es Salaam kuna shule ya msingi iliyopewa jina lake pia. Shule hii ilianzishwa mwaka 2002 baada ya serikali kugawanya Shule ya Msingi Mapambano na kuwa shule mbili; Mapambano na Shekilango.

Kwa kuwa wakati huo ajali hiyo ya ndege ilipotokea na kusababisha kifo cha Shekilango na wengine, ujenzi wa Barabara ya Sinza (ilivyouwa ikiitwa kabla) ndio ulikuwa umeanza, uongozi wa Jiji la Dar es Salaam ukaamua kumuenzi Shekilango kwa kuipa barabara hiyo jina lake.

Shekilango aacha mjane

Kifo cha Shekilango kilisababisha mke wake kuwa mjane na kuacha watoto wanne ambao ni Mussa, Suleiman, Salama na Mambiu. Mke wake alikuwa mwalimu maarufu Dar es Salaam na alijuliana zaidi kwa jila la Mwalimu Zippora.

Mwalimu Zippora, aliyezaliwa mwaka 1938, alikuwa hodari aliyefundisha shule nyingi za sekondari nchini. Ni mwalimu aliyekuwa na heshima hadi kufikia wadhifa wa kuwa mwalimu mkuu wa shule nyingi za sekondari zikiwamo Zanaki, Kisutu, Forodhani, Jangwani, Msalato na Shule ya Wasichana Iringa.

Baadaye, kutokana na juhudi zake, alipewa dhamana ya kuwa Ofisa Elimu wa Jiji la Dar es Salaam na baadaye kuhamishiwa Wizara ya Elimu ambako alikuwa akiongoza kitengo kilichokuwa kikisimamia elimu ya sekondari nchini Tanzania.

Mwalimu Zippora alifariki dunia Septemba Mosi, 2018 na kuzikwa Jumamosi Septemba 8, 2018 huko Mombo, Tanga.



Sehemu ya Barabara ya Shekilango?

Tangazo

Tangaza na Pambazuko

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.



Kwa bei nafuu sana

0744 768 263 au Barua-
Pepe; info@pambazuko.tz

Akutana na 'vijana wake' wa JKT baada ya miaka 30



Baadhi ya waliofuzu mafunzo ya mwaka mmoja katika Jeshi la Kujenga Taifa, Kambi ya Bulumbora, Kigoma, wakiwa katika picha ya pamoja na msaidizi wa mkuu wa kambi hiyo, Meja (mstaafu) Christopher Mzena, waliyeonana mara ya mwisho miaka 30 iliyopita.



Vulifrída Malya, kushoto, akisalimiana na aliyekuwa msaidizi wa mkuu wa kambi ya JKT Bulumbora, Meja (mstaafu), Christopher Mzena.



Mwenyekiti wa Umoja wa Waliofuzu Bulumbora JKT - 1993, Magayane Machibya (katikati) akisalimiana na aliyekuwa msaidizi wa mkuu wa kambi hiyo, Meja (mstaafu) Christopher Mzena, waliyeachana miaka 30 iliyopita. Kushoto ni katibu wa umoja huo, Clement Kitandala. (Picha sote na mpigapicha wa Pambazuko).

Na Mwandishi WETU

JUMAMOSI iliyopita – Mei 13 ilikuwa siku ya furaha kwa baadhi ya wahitimu wa mafunzo ya kijeshi kutoka Kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Bulumbora, Kigoma waliokutana na aliyekuwa msaidizi wa mkuu wa kambi hiyo, Meja (mstaafu) Christopher Mzena.

Furaha hiyo ilionekana “kujaa” kwenye nyuso za waliokuwepo kwenye hafla fupi iliyoandaliwa na uongozi wa umoja wa wana JKT hao walioko Dar es Salaam.

Mwenyekiti wa umoja huo, Machibya Magayane alisema pamoja na taarifa fupi kwa wanachama walioko Dar es Salaam, lakini anaamini hata waliokwama kuhudhuria, walikuwa na furaha kuu kushuhudia wenzao wakiwakilisha kukutana na kiongozi aliyewalea wakati wakiwa JKT.

Meja (mstaafu) Mzena hakuficha furaha yake kwa kukutana na vijana wake ambao wengi aliwasahau, hadi walipoeleza baadhi ya “vituko na matukio” ambayo walihusika nayo wakiwa jeshini, hata kuffika ofisini kwake kwa uamuzi wa kijeshi.

Buriani

Kwaheri Bernard Kamilius Membe



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, jana ameongosa waambolezaji katika kuuaga mwili wa aliyewahi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Tanzania, Bernard Membe katika Viwanja vya Karinjee, Dar es Salaam. Membe alifariki dunia Mei 12 na atasikwa kesho kijijini kwake Rondo, Lindi. (Picha na Ikulu)





Kikosi cha Yanga

Yanga wasibweteke Afrika Kusini

Na Mwandishi WETU

MABINGWA wa Soka Tanzania, Yanga ambao sasa wanakabiliwa na kibarua kigumu cha kuhakikisha wanatinga fainali za michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, wameshauriwa kuongeza kasi, ujuzi wa kufunga mabao mapema, ulinzi imara wakati watakapokuwa wakicheza na Marumo Gallants ya Afrika Kusini.

Mechi ya marudiano kwa timu hizo inatarajiwa kucheza nchini Afrika Kusini wiki hii, ambapo Yanga itahitaji ushindi, suluhu ama sare ya magoli yoyote kuweza kufuzu kuingia kwenye kipute cha fainali.

Katika mechi wa kwanza iliyochezwa Dar es Salaam, Tanzania na Yanga kuibuka kidedea kwa mabao 2-0, bado mashabiki na wachambuzi wa soka wanaeleza kutoridhishwa na kiwango cha mpira uliochezwa na Yanga dhidhi ya wapinzani wao, Marumo.

Mchambuzi wa mpira wa miguu kutoka Morogoro, Simon Kehehah, ambaye alikuwepo uwanjani wiki iliyopita kushuhudia mchezo huo, alisema pamoja na Yanga kushinda, haikuonyesha kiwango chake kikubwa kama ilivyotarajiwa.

“Yanga pamoja na furaha ya magoli,

lakini kiwango chake hakikuwa kikubwa, wachezaji wake walionekana kutofungamana kwa kasi, ujuzi kiasi kwamba mipira haikufika haraka mbele kwa wafungaji, hali ambayo iliwafanya washindwe kupata mabao ya awali,” alisema mchambuzi huyo.

Akaongeza kwamba Yanga wanapaswa kujifua zaidi kwa siku hizi zilizobaki na kuwa na “pumzi zaidi” kwani wapinzani wao wanaonekana kuwa na nguvu na uwezo mkubwa wa kukimbia na kukaa bila kuchoka.

Ali Hamis, ambaye ni shabiki wa Yanga kutoka Dar es Salaam, anasema Marumo ni timu ambayo haipaswi kwenda “kuichekea, ni lazima ifungwe mapema” na kwamba wachezaji wa timu hiyo ya Afrika Kusini wanajituma zaidi.

“Hawa jamaa wa Afrika Kusini, ni hatari sana, wanaweza kukimbia na hawachoki na wana uwezo mkubwa wa kukaa na mpira, hivyo Yanga waende vitani na wasiwe na akili ya kwenda kuokota ushindi, wakapambane hasa,” anaongeza Ali.

Mchezo wa timu hizo mbili unatarajiwa kufanyika wiki hii na kwamba Yanga wamewasili Afrika Kusini kwa ajili ya mechi ya marudiano.

Inatafakarisha...



Mwalimu wa Shule ya Msingi Siyiape iliyoko Kaunti ya Narok, Kenya akishikiza uzi kwenye sare ya mwanafunzi. Inadaiwa kuwa mwanafunzi huyo anatoka familia isiyokuwa na uwezo mkubwa, hivyo binti yao kuvaa sare iliyochanika. Picha hii iliyosambaa kwenye mitandao ya kijamii, hatimaye ilimfikia mwanasiasa machachari wa Nairobi, Mike Sonko ambaye baadaye alinunua sare tano za shule na viatu jozi tano kwa mwanafunzi huyo.

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.